

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

Telegramu "NISHATI".
Simu: (255)-26-2322018
Nukshi: (255)-26-2320148
Barua Pepe: ps@nishati.go.tz



Mji wa Serikali -Mtumba,
Mtaa wa Nishati,
S. L. P. 2494,
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kutokana na kuendelea kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia kunakosababishwa na mambo mbalimbali ikiwemo vita kati ya Urusi na Ukraine, mwenendo wa bei za mafuta nchini umeathirika kwa bei hizo kuendelea kupanda.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali kuitia Wizara ya Nishati imeondoa **Tozo ya Shilingi 100 kwa kila lita** ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa, zilizopaswa kulipwa na watumiaji wa mafuta nchini kwa muda wa **miezi mitatu** zaidi kuanzia mwezi Machi 2022 hadi Mwezi Mei 2022 huku ikiendelea kutathmini mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia.

Pamoja na kwamba uamuzi huu utaipunguzia Serikali mapato ya kiasi cha **Shilingi billioni 30** kwa mwezi, Serikali imeona ni muhimu kuendelea kuwalinda wananchi wake dhidi ya athari za mabadiliko ya bei za mafuta ulimwenguni. Hii inatokana na ukweli kwamba endapo uamuzi huu usingechukuliwa na Serikali, bei za mafuta nchini kuanzia mwezi Machi na kuendelea zingekuwa za juu sana kutokana na sababu zilizolezwu hapo juu.

Kwa msingi huo, **Mheshimiwa January Makamba (Mb), Waziri wa Nishati**, ameidhinisha na kusaini marekebisho ya kanuni inayohusika na Tozo hiyo ili kutimiza uamuzi huu wa Serikali.

Uamuzi huu unaenda sambamba na maelekezo ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, aliyoyatoa baada ya kikao na Wizara na taasisi mbalimbali zinazohusika na suala hilo zilizokutana tarehe 5 Oktoba 2021 kujadiliana namna bora ya kupunguza bei za mafuta hapa nchini na kupunguza tozo mbalimbali zenyeh thamani ya **Shilingi billioni 102** kwa watumiaji wa mafuta nchini

Bei mpya za mafuta zitakazotangazwa na EWURA na kuanza kutumika tarehe 2 Machi 2022 zitazingatia marekebisho hayo ya kanuni yaliyofanywa na Waziri wa Nishati.

IMETOLEWA NA:

WIZARA YA NISHATI

28.02.2022